



FUNGAMANO
LA MAKANISA
YA KILUTHERI
DUNIANI

FUNGAMANO LA MAKANISA YA KILUTHERI DUNIANI (FMKD-LWF)

Maombezi juu ya mlipuko wa COVID-19 (Corona Virus)

Ee Mungu Mponyaji, onesha huruma yako kwa wanadamu walio katika taharuki na kulemewa na magonjwa na hofu. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Uwe msaada wetu hasa wakati huu ambapo virusi vya Corona vinazidi kusambaa ulimwenguni, uponye wagonjwa, uzisaidie na kuzilinda familia zao na marafiki ili wasiathirike. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Utupe roho ya upendo na nidhamu binafsi ili tushikamane kwa pamoja kuzuia na kutokomeza virusi vya Corona. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Tuwezeshe tuwe makini na mstari wa mbele katika kutokomeza magonjwa yote, malaria, dengue, VVU/UKIMWI, na mengine (yanaweza kutajwa kwa sauti au kimya)... yanayosababisha mateso na hata kifo kwa watu wengi. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Utuponye na kujipenda wenyewe kunakotufanya tuogope pale tu virusi vinapokuwa tishio kwetu, fungua njia pale mashaka na hofu vinafanya tusiwajali majirani zetu. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Waimarishe na kuwatia moyo wanaotoa huduma ya afya ya msingi kwa jamii na wataalamu wote wa afya: wauguzi, madaktari, wote wanaojitoa kuhudumia wagonjwa na familia zao. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Watie moyo na uwape tumaini wote wanaofanya utafiti kwa ajili ya kupata chanjo ya virusi vya Corona. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Waimarishe wafanyakazi na wafanya biashara wote waliopata hasara kwa kupoteza kipato kwa sababu ya kufungwa kwa shughuli za biashara, karantini, kufungwa kwa mipaka na vizuizi vingine... walinde na kuwahifadhi wote ambao wanalazimika kusafiri. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Waongoze viongozi wa mataifa mbalimbali ili waseme kweli, kuzuia kusambaa kwa taarifa zisizo sahihi na kutenda kwa haki ili familia na jamii yako yote iujue uponyaji wako. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Ponya dunia, uiponye miili yetu, utupe nguvu katika mioyo yetu na akili zetu, na katika janga hili utupe tumaini na amani. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Katika upendo wako uwapokee wale wote waliofariki na wale watakaofariki leo. Uwafariji wapendwa wao katika huzuni yao. Ee Mungu, sikia kilio chetu.

Usikie kuomba kwetu.

Katika upendo wako, uikumbuke jamaa ya watu wako wote na uumbaji wako.

Amen!